

SEHEMU YA SITA

AMANI NA UTULIVU BUNGENI

58.-(1) Bila ya kuathiri masharti ya Kanuni ya 4(2), Spika, atawajibika kuhakikisha kuwa utaratibu bora unafuatwa Bungeni, na uamuzi wake kuhusu jambo lolote la utaratibu utakuwa ni wa mwisho.

Spika
kuisisitiza
utaratibu
ufuatwe

(2) Mbunge yeyote atakayekiuka utaratibu au Kanuni za Bunge anaweza papo hapo kutakiwa na Spika, afuate utaratibu; na vile vile Mbunge mwingine yeyote aweza kusimama na kumfahamisha Spika kwamba kuna Mbunge anayekiuka utaratibu.

Adhabu
kwa
Mbunge
anaye-
kiuka
Kanuni

59.-(1) Mbunge anayeshikilia kusema mambo ambayo

hayaruhusiwi na Kanuni hizi, aweza kuamriwa na Spika akatishe hotuba yake na kurejea kukaa mahali pake.

Adhabu
zinazo-
weza
kutolewa
na Spika

(2) Iwapo Mbunge yeyote atatumia maneno au lugha isiyotakiwa Bungeni, kwa mfano lugha ya matusi, ya usafihi, ya uchokozi au ya kumuudhi Mbunge mwingine, na kama akitakiwa kujirekebisha kwa kufuta usemi wake huo atasita au atakataa kufanya hivyo, basi Spika, aweza kumwamuru Mbunge huyo atoke mara moja nje ya Ukumbi wa Bunge, na abaki huko nje kwa muda wote uliosalia kwa kikao cha siku hiyo.

(3) Iwapo hadi kufikia mwisho wa muda aliopewa, Mbunge aliyeaniwa kuthibitisha ukweli wa usemi wake kwa mujibu wa Kanuni ya 50(1) atakataa au atashindwa kutoa uthibitisho huo kwa kiwango cha kuliridhisha Bunge, basi Mbunge huyo atachukuliwa hatua na Spika kwa, mujibu wa Kanuni ya 59(2). Lakini endapo Mbunge mwingine yeyote ataona kwamba uwongo uliosema na Mbunge huyo ni mkubwa kiasi cha kuathiri heshima ya Bunge, aweza papo hapo kutoa hoja kwamba Mbunge huyo asimamishwe kazi za Bunge kwa kipindi maalum atakachokitaja katika hoja yake. Hoja ya aina hiyo yaweza kutolewa bila taarifa, na itajadiliwa na kuamuliwa kama hoja nyingine yoyote. Kama kuna hoja nyingine inayojadiliwa wakati huo, basi hoja ya kumsimamisha Mbunge huyo aliyetajwa itatolewa mara baada ya hoja iliyokuwa ikijadiliwa kuamuliwa.

60.-(1) Endapo Mbunge yeyote ataonyesha kutojali mamlaka ya Spika, na kuendelea kuvuruga mwenendo bora wa shughuli za Bunge, basi Spika, aweza kumtaja Mbunge huyo kwamba amedharau mamlaka ya Spika. Papo hapo Mbunge mwingine yeyote aweza kutoa taarifa ya mdomo kwa kutumia Kanuni ya 51 (1), kwamba anakusudia kutoa hoja baadaye, ya kumsimamisha kazi Mbunge huyo aliyetajwa. Mbunge aliyetoa taarifa hiyo atapewa nafasi ya kutoa hoja yake mara baada ya hoja iliyokuwa ikijadiliwa kuamuliwa, na hoja hiyo itajadiliwa na kuamuliwa kama hoja nyingine yoyote. Kama kosa limetendeka, katika Kamati ya Bunge Zima, basi papo hapo Mwenyekiti atasimamisha shughuli za Kamati hiyo, Bunge litarudia na Mwenyekiti atatoa taarifa kwa Bunge kuhusu mwenendo wa Mbunge mhusika. Baada ya hapo utaratibu utakuwa kama ilivyokwisha kuelezwa katika fasili hii.

Adhabu
zinazo-
weza
kutolewa
na Bunge

(2) Kama hoja yoyote chini ya fasili hii itapitishwa na Mbunge kusimamishwa kazi, basi ikiwa ni kosa lake la kwanza ataendelea kuwa ameendelea kusimamishwa hadi kikao cha tano, kama kosa la pili hadi

kikao cha ishirini, lakini kama kosa ni la tatu au zaidi basi Mbunge huyo ataendelea kuwa amesimamishwa kazi hadi hapo Bunge litakapoamua kwamba kusimamishwa huko kwa Mbunge kukome.

(3) Bila kujali masharti ya fasili zilizotangulia za Kanuni hii, Bunge laweza kumchukulia hatua nyinginezo za kinidhamu Mbunge yeyote aliyetenda kosa chini ya Kanuni hizi, kwa kumpitishia azimio ambalo litataja hatua hizo zinazokusudiwa kuchukuliwa, pamoja na sababu zake.

61. Mbunge aliyesimamishwa kazi kwa mujibu wa Kanuni ya 59(3) au ya 60(2) atatoka katika Bunge na hataingia tena katika sehemu yoyote ya Ukumbi wa Mikutano ya Bunge kwa muda wote atakapokuwa amesimamishwa, na atalipwa nusu mshahara na nusu posho zozote zinazoambatana na mshahara huo.

Masharti
kwa
Mbunge
aliyesima-
mishwa
kazi

62. Kwa madhumuni ya kudhibiti fujo, endapo itatokea ndani ya Ukumbi wa Bunge, na Spika ataona kuwa kuna haja ya nguvu kutumiwa, basi Spika, aweza kuahirisha Bunge bila ya hoja yoyote kutolewa au kusimamisha kikao kwa muda ambao yeye atautaja ili fujo hiyo iweze kudhibitiwa na vyombo vya dola.

Kukitokea
fujo